Muhimu

Kwa ushauri zaidi kuhusu huduma inayokufaa, zungumza na mtoa huduma aliye karibu nawe!

"Nina ufahamu wa kutosha kuhusu huduma za afya ya uzazi. Najipanga nifanikiwe!"



Kwa maelezo zaidi tembelea kituo cha huduma za afya kilicho karibu nawe

au

Tupigie 0800750360

Imetolewa na
Wizara ya Afya

Tunampa mtoto nafasi ya kukua



Unachohitaji kufahamu kuhusu huduma za Afya ya Uzazi kabla na baada ya Ujauzito.

“Unafikiria kupishanisha mtoto wako ajaye? Hongera!”

Kipeperushi hiki kitakupa taarifa muhimu kuhusu jinsi ambavyo huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya ujauzito zinakuwezesha kufikia malengo yako.

Fahamu kuhusu huduma za afya ya uzazi

Mamilioni ya wanawake duniani hutumia huduma hizi kupishanisha watoto.

- Wanawake wengi wanazitumia kupishanisha ama kupanga idadi ya watoto wanaowahitaji.
- Huduma hizi ni salama na zina ufanisi mkubwa katika kuzuia ujauzito usio tarajiwa.
- Mtoa huduma za afya atakupa ushauri kukuwezesha kuchagua njia inayokufaa.
- Huduma hizi haziathiri uzazi kwani ukiacha kuzitumia tu, unarejea katika hali ya kuweza kupata mtoto.

ZIMETHIBITISHWA!

Je, mwenzi wako anafahamu jinsi huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya kujifungua zinavyoweza kuinufaisha familia yako?

- Zinawawezesha kujipanga na kuamua lini mpate mtoto.
- Zinalinda afya ya mama.
- Zinampa mtoto fursa ya kukua kimwili na kiakili.
- Zinailetea familia yako mafanikio, kwani kusubiri kwa miaka miwili au zaidi kunawapa muda, nafasi na fursa ya kufikia malengo yenu.

Taarifa kuhusu huduma za afya ya uzazi kwa wanaume

- Wanaume wengi hushirikiana na wenzi wao kutumia huduma hizi.
- Wanawake wanaojadili matumizi ya huduma hizi na wenzi wao hujihisi wanapendwa zaidi.

Je, kwa nini wanaume wanapaswa kuunga mkono matumizi ya huduma za afya ya uzazi?

- Wataheshimiwa na jamii na wanaume wenzao.
- Wataonekana kama mfano wa kuigwa.
- Watachangia kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi na kuimarisha afya ya mama na mtoto.

KUMBUKA:
Huduma hizi ni salama na zimethibitishwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi

- Huduma hizi hupatikana bila malipo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.
- Watoa huduma za afya huhakikisha huduma inatolewa katika mazingira ya faragha na usiri.
- Kwa maeneo yasiyofikika kirahisi, huduma hizi zinakufikia kwa njia ya huduma za mkoba.
- Kuna njia mbalimbali za afya ya uzazi zinazompa mama wigo wa kuchagua inayomfaa kulingana na mahitaji yake.
- Huduma za afya ya uzazi kabla na baada ya ujauzito ni haki yako. Wewe ndiye mwenye maamuzi ya mwisho ya kuzitumia.

